JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

Simu: +255262963470
Nukushi: +255262963117
Barua pepe: [ps@mit.go.tz](mailto:ps@mit.go.tz)
Tovuti: [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S. L. P 2996,
**40478 DODOMA**.

## TAARIFA KWA UMMA

## MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA MUHIMU NCHINI KWA MWEZI FEBRUARI 2023

### 1. UTANGULIZI

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaendelea kufanya tathmini ya mwenendo wa bei za mazao ya chakula na bidhaa muhimu nchini kwa lengo la kutoa taarifa kwa Wananchi kuhusu mwenendo wa bei nchini. Taarifa hizi ni muhimu kwa ajili ya kuwawezesha wadau ikiwa ni pamoja na wazalishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali, watumiaji wa bidhaa hizo, wenye viwanda na wafanyabiashara kupata taarifa ili kufanya maamuzi yatakayochangia kukuza uchumi na kipato katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Wizara inaendelea kuratibu ukusanyaji wa takwimu za bei za mazao na bidhaa muhimu kama vile vyakula na vifaa vya ujenzi kutoka kwenye masoko yaliyopo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia Wakusanya Taarifa za Masoko (Market Monitors) na Maafisa Biashara wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Takwimu hizi husaidia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) katika ukokotoaji wa kiwango cha mfumuko wa bei kila mwezi na kuweza kufanya tathmini ya upatikanaji wa mazao na bidhaa mbalimbali nchini.diliko

### 2. MWENENDO WA BEI ZA MAZAO NA BIDHAA ZA VYAKULA

#### i. Mahindi

Bei ya mahindi kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 750 na 1,750 kwa kilo. Bei ya chini haijaonyesha mabadiliko wakati bei ya juu imepanda ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari, 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 750 na 1600 kwa kilo. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Iringa, Songwe, Njombe na Ruvuma na kwenye maeneo yote

ambayo Serikali imepeleka mahindi ya bei ya ruzuku, wakati bei ya juu ipo katika Mikoa ya Kigoma, Mara na Lindi. Aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na ongezeko hili la bei ikiwa ni pamoja na kufungua vituo vya kuuzia mahindi katika mikoa 15 na halmashauri mbalimbali nchi nzima kwa wastani wa bei ya Shilingi 680 hadi 900 kwa kilo ambapo hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2023 jumla ya tani 29,084 zimeshaingizwa sokoni.

### ii. Unga wa Mahindi

Bei ya Unga wa mahindi kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 1,500 na 2,100 kwa kilo. Bei ya unga wa mahindi haijabadilika ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Geita na Manyara na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Kigoma na Mara.

### iii. Mchele

Bei ya mchele kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 2,500 na 3,500 kwa kilo. Bei ya mchele haijabadilika ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023. Mikoa yenye bei ya chini ni Iringa, Simiyu na Tabora na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Manyara. Aidha, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ongezeko la bei ya mchele ikiwa ni pamoja na kutoa vibali vya kuingiza mchele kutoka nje ya nchi ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya tani 90,000 za mchele zinatarajiwa kuingia sokoni na hivyo kushusha bei.

### iv. Maharage

Bei ya maharage kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 2,300 na 4,000 kwa kilo. Bei ya chini imeshuka ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 2,400 kwa kilo. Bei ya chini inapatikana katika Mkoa wa Songwe na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Shinyanga.

### v. Viazi Mviringo

Bei ya Viazi Mviringo kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 1,000 na 1,750 kwa kilo. Bei ya chini imepanda ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 800 kwa kilo, Bei ya juu ya Viazi Mviringo imeshuka ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 2,000. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Songwe,Tanga na Mbeya na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Manyara, Mara na Ruvuma.

### vi. Unga wa Ngano

Bei ya unga wa ngano kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 2,000 na 2,500 kwa kilo. Bei ya juu ya unga wa ngano imeshuka ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 3,200 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika maeneo mengi nchini na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Songwe.

### vii. Sukari

Bei ya sukari kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 2,700 na 3,000 kwa kilo. Bei hiyo imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na mwezi Januari, 2023. Hali hiyo inatokana na jitihada zinazoendelea za kuvutia uwekezaji na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa sukari nchini. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Pwani na Singida na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Ruvuma, Manyara na Lindi.

### viii. Mafuta ya Kupikia

Bei ya mafuta ya kupikia ya Alizeti kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 4,750 na 7,800 kwa lita. Vile vile, bei ya mafuta ya kupikia ya Mawese (Korie na Safi) ni kati ya Shilingi 4,500 na 7,250 kwa lita. Bei ya mafuta ya kupikia imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na mwezi Januari, 2023. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya Alizeti ipo katika Mikoa ya Manyara, Morogoro na Singida na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Lindi, Pwani, Mtwara na Mara.

## 3. MWENENDO WA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI

Bei za vifaa vya ujenzi kwa mwaka 2023 zimeendelea kushuka kutokana na kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa hizo sambamba na usimamizi madhubuti wa mwenendo wa soko la bidhaa hizo uliofanywa na Wizara na taasisi zake.

### i. Saruji

Bei ya saruji kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 14,750 na 23,500 kwa mfuko wa kilo 50. Bei hiyo imeshuka ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023. Mikoa yenye bei ya chini ni Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Pwani na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Mara, Kigoma na Katavi.

### ii. Nondo

Bei ya nondo mm 10 kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 16,100 na 25,000. Bei ya chini imeshuka ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 17,500. Bei ya juu ya nondo mm 10 imepanda ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 23,000. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Iringa, Mwanza na Tanga na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Lindi.

Bei ya nondo mm 12 kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 22,000 na 28,000. Bei ya chini imeshuka ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 23,000 kwa nondo. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Katavi.

### iii. Bati

Bei ya bati nyeupe geji 30 kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 22,000 na 30,000. Bei ya chini ya bati imepungua ikilinganishwa na bei ya mwezi Januari, 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 22,500. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Tanga, Songwe,Kilimanjaro Singida na Ruvuma na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Njombe.

## 4. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA NYINGINE

### i. Sabuni

Bei ya Sabuni aina ya Jamaa, White wash na MO kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 2,500 na 4,000 kwa mche. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Simiyu na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Mbeya.

Bei ya Sabuni aina ya Takasa, kiboko na Kuku kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 1,200 na 3,250 kwa mche. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Mara na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Ruvuma na Tanga.

Bei ya Sabuni za Magadi kwa mwezi Februari ni kati ya Shilingi 1,000 na 3,250. Sabuni za magadi zipo aina mbili nazo ni miche myembamba na miche minene. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Dodoma na Mara.

## 5. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA ZA VYAKULA KWA NCHI JIRANI

Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake kwenye kiasi cha mavuno ya mazao muhimu ya chakula kama mchele, mahindi, maharage na viazi mviringo, mahitaji ya bidhaa hizo kwenye nchi jirani yamekuwa makubwa kuliko uzalishaji hivyo, kuchangia kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula nchini na nchi jirani.

Aidha, kwa ujumla bei za vyakula katika nchi nyingi duniani zimepanda. Hata hivyo, mfumuko wa bei nchini Tanzania ni wa kiwango cha chini zaidi ikilinganishwa na nchi jirani ambapo kwa Tanzania kiwango cha mfumuko wa bei ni asilimia 4.9 kwa mwezi Januari 2023 ikilinganishwa na asilimia 9.1 ya Kiwango cha mfumuko wa bei nchini Kenya , asilimia 10.4 nchini Uganda na asilimia 21.7 nchini Rwanda kwa mwezi Januari, 2023.

## 6. HITIMISHO

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Ninapenda kuhitimisha taarifa yangu kwa kuuhakikishia umma wa Watanzania kuwa, Serikali inaendelea kufuatilia na kufanya tathmini ya bei za bidhaa muhimu ili kulinda maslahi ya wadau wote ikiwa ni pamoja na wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa husika. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwahimiza Wafanyabiashara kote nchini kuendelea kuzingatia misingi ya ushindani wa haki katika kufanya biashara ili kuunga mkono jitihada za Serikali za kukuza uchumi kwa manufaa ya Wananchi wote. Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ushindani Namba 8 ya mwaka 2003 na Kanuni za Ushindani za mwaka 2018 kwa lengo la kumlinda mlaji na kushajihisha ushindani. Vilevile, Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa muhimu na mazao ya chakula ili kudhibiti mfumuko wa bei nchini.

Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa taarifa za uhakika za bei za bidhaa na masoko, kufanya uchambuzi na kusambaza kwa wadau. Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia Idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyoanzishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini ili tupate taarifa za kuaminika na kwa wakati kutoka maeneo yote nchini. Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza Maafisa Biashara kote nchini kwa kushirikiana na Maafisa Ugani waliopo katika maeneo yao kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu uzalishaji wa bidhaa hasa za kilimo pamoja na mwenendo wa bei katika maeneo wanayosimamia ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa za bei na kuziwasilisha kwa wakati Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Nitoe rai kwa wazalishaji wa bidhaa zote za viwandani kuongeza jitihada za uzalishaji wa bidhaa na kwa ubora unaohitajika sokoni. Kumekuwepo na malalamiko ya watuamiaji wa bidhaa zetu za viwandani kuhusu ujazo na hata ubora wa bidhaa hizo. Niwatake Wakala wa Vipimo Tanzania kufanya Ufuatiliaji wa karibu juu ya malalamiko haya na hatua madhubuti zichukuliwe kwa wote Watakaopatikana na kosa la kuzalisha bidhaa chini ya kiwango na ujazo unaohitajika na ulioonyeshwa kwenye vifungashio.

Tunaelekea kuanza mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Kwaresma, ni matarajio ya Serikali kwamba bei ya bidhaa zote zinazotumika kwa wingi kwenye kipindi hiki hazitopanda. Ndugu zangu Wazalishaji wa sukari, tumekuwa na vikao vya pamoja na kwa umoja wetu tumekubaliana tuna sukari ya kutosha ndani ya nchi yetu hivyo hatutarajii kuona bei ya sukari inapanda Aidha bei ya Unga wa ngano imeonyesha kushuka ndani ya miezi hii miwili, hivyo hatutarajii kuona ikipanda tena kwani Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuwa na bidhaa hii ya kutosha ndani ya nchi yetu. Hali kadhalika, yapo maeneo ndani ya Nchi yetu wameanza kuvuna maharage maana yake hatutarajii kuona bei ya bidhaa hii muhimu ikipanda tena. Vimetolewa vibali vya kuingiza Nchini mchele tani 90,000 ambazo zitaanza kuuzwa kwa bei elekezi ya Serkali ndani ya Mwezi wa Tatu, hivyo kwenye bidhaa hii nayo tunatarajia bei itashuka ndani ya wiki mbili zijazo. Niendelee kuwahakikishia Watanzania wote kwamba, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti kwenye maeneo yote ambayo yanaonekana kuchangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei ili tuendelee kubaki kwenye wigo wa

mfumuko wa bei tuliokubaliana ndani ya Nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

…………………………………………………………

**Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb)**

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

**FEBRUARI, 2023**